**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OR-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO**

# UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA MAFANIKIO KATIKA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE CHINI UONGOZI WA MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**MS. FATUMA O. LATU**



**UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ni moja kati ya Halmashauri **9** katika Wilaya **7** za Mkoa wa Pwani ambayo ilianzishwa mwaka **1962**, ikiundwa na Tarafa **2**, Kata **11**, Vijiji **8** na Vitongoji **174.** Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao **109,633** ambapo Wanaume **54,562** na wanawake **55,071.**

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ipo katika ukanda wa Pwani ikiwa na ukubwa wa Kilomita za Mraba **945,** Makao makuu ya Halmashauri yakiwa Bagamoyo mjini, Mji maarufu wenye historia ya kipekee ya mali kale za majengo ya zamani na historia ya biashara ya watumwa.

Kijiografia, Mji wa Bagamoyo upo umbali wa kilomita **65** kaskazini ya jiji la Dar es Salaam, ambapo hali ya hewa ya Mji wa Bagamoyo ni yakitropiki, yenye joto la kadri. Kiwango cha juu cha joto ni nyuzi joto **$30^{0}$C** na kiwango cha chini ni nyuzi joto **$13^{0}$C**. Halikadharika, Halmashauri inapata mvua kiasi cha wastani wa **mm 800 – mm1200** kwa Mwaka.

**SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

Shughuli kuu za kiuchumi zinazotegemewa na Wananchi wa Bagamoyo ni Uvuvi, Kilimo, Utalii, Uchimbaji Madini, Ufugaji pia shughuli za biashara na viwanda.

**MIAKA MINNE YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI BAGAMOYO**

Katika kipindi cha Miaka minne ya Uongozi wa Mhe. Rais John Pombe Joseph Magufuli, Bagamoyo chini ya uongozi mahiri wa Mkurugenzi Mtendaji, Bi. Fatuma O. Latu, imepiga hatua kubwa ya maendeleo baada ya Serikali kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo iliyotatua kero za Wananchi kwa kiasi kikubwa kama si kuzimaliza kabisa.

Miradi hii ya maendeleo imetekelezwa katika Sekta za Afya, Elimu, Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, na Maendeleo ya jamii ambapo, imeibadilisha kabisa Bagamoyo ya sasa kwani, imesogeza huduma za Kijamii karibu na Wananchi na kutatua kero zilizokuwa zikisumbua Wananchi kwa muda mrefu.

Bi. Fatuma O. Latu, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, aliteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mnamo Mwezi Septemba, 2016 na katika kipindi cha uongozi wake kama Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hii, amesimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo yenye tija, iliyotekelezwa na Serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Miradi hii ililenga kuondoa kero za Wananchi na kuwaletea wana Bagamoyo maendeleo chanya.

**SEKTA YA AFYA**

Kabla Wilaya ya Bagamoyo haijagawanywa katika Halmashauri mbili, yaani Halmashauri ya Chalinze na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Wilaya ilikuwa na vituo vinne vya Afya katika Kata ya Chalinze, Lugoba, Miono na Mbwewe.

Baada ya mgawanyo, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo haikuwa na Kituo cha Afya hata kimoja, kwani vituo vyote vinne vya Afya vilibaki katika Halmashauri ya Chalinze Kiutawala.

Kadhalika, Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ilibaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, na kwakuwa hakukuwa na kituo cha Afya hata kimoja, hali hii ilipelekea

utoaji huduma katika Hospitali ya Wilaya kuwa mgumu kutokana na kuzidiwa na msongamano wa wagonjwa, toka katika Kata zote 11 za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Sekta ya Afya katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Mhe Rais. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imepiga hatua kubwa ya mafanikio kwa kuondoa kero na changamoto za kukosa huduma bora na za uhakika za Afya, hasa Afya ya Mama na mtoto karibu na Wananchi.

Wananchi walilazimika kuifuata huduma hii mbali na maeneo wanayoishi, hali iliyopelekea wakina mama wengi kupoteza maisha wakati wa Kujifungua, kwa kujifungulia majumbani na kukosa huduma za wataalamu wa Afya, ama kwa kujifungulia njiani wakiwa wanafuata huduma za Afya mbali na maeneo wanayoishi.

Mwaka **2017,** Mwezi Julai, Halmashauri ilipokea kiasi cha Shilingi **Milioni 500** kutoka Serikali Kuu, kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ambazo zilielekezwa katika Ujenzi wa Kituo kipya cha Afya Kerege, kilichopo Kata ya kerege, Wilayani Bagamoyo.

**UTEKELEZAJI WA MRADI**

Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kerege ulianza rasmi, **tarehe 20/10/2017** na ulikamilika tarehe **15/01/2018** ambapo ulitekelezwa kwa njia ya ***'force account',*** huku lengo kuu la mradi likiwa ni Uboreshaji vituo vya Afya Nchini na kuvifanya kuwa vyenye ufanisi.

Majengo ya kipaumbele katika mradi huu yalikuwa,
- i) Jengo la upasuaji;
- ii) Jengo la wazazi;
- iii) Nyumba ya Mtumishi;
- iv) Jengo la maabara.

Hadi kukamilika kwa mradi huu, kulikuwa na nyongeza ya majengo 6 ambayo ni Jengo la kuhifadhia maiti (mortuary), Jengo la kufulia (laundry), Jengo la kuchomea taka (incinerator), Jengo la kupokelea umeme (power house), Mnara (tanki lita 10000) wenye choo na stoo na Mnara (tanki lita 3000) wenye choo tundu moja.

Majengo haya yote 6 ya nyongeza yalijengwa kwa kutumia fedha zilizopokelewa awali yaani Shilingi Milioni 500 toka Serikali kuu na Mchango toka Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo Shilingi **Milioni 44** toka katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani. Kukamilika kwa Kituo cha Afya Kerege kumesaidia Wananchi takribani **7114** wa Kata ya Kerege na Kata jirani, ambapo huduma zote muhimu za Afya zinapatikana katika Kituo hicho.

Lengo la Serikali ni kuhakikisha Afya ya Mama na Mtoto inabaki salama, hasa wakati wa kujifungua na huduma hiyo kupatikana karibu na Wananchi ili kuepuka vifo vinavyoweza kutokea wakati wa kujifungua.

**MAFANIKIO YA MRADI**

Kituo cha Afya Kerege ambacho kimejitosheleza kimiundombinu, wataalamu wa Afya na vifaa tiba, kilianza kutoa huduma rasmi Mwezi **Oktoba 2018** na hadi sasa jumla ya

kinamama 941 wamejifungua salama Kituoni hapo, ambapo wakina mama 89 walijifungua kwa njia ya upasuaji.

Aidha, Serikali ilipeleka vifaa tiba toka Mamlaka ya Dawa (MSD) ambavyo vimekuwa chachu ya ufanikiwaji wa mradi huu katika kutoa huduma bora kwa Wananchi.

**MWONEKANO WA KITUO CHA AFYA KEREGE**









***Huduma zikiendelea kutolewa katika kituo cha Afya Kerege***

Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kerege ulikuwa ni wa mafanikio makubwa kwani kituo hiki kilishika nafasi ya kwanza kwa ubora Kitaifa kati ya Vituo vya Afya vilivyojengwa na fedha kutoka Serikali kuu katika Mwaka wa fedha 2017/2018.

Ufanisi wa utekelezaji wa mradi wa Kituo cha Afya Kerege, ulipelekea Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kuongezewa fedha kiasi cha Shilingi **Milioni 400** toka Serikali kuu, kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, fedha zilizoelekezwa katika utekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Pili kipya cha Afya Matimbwa kilichopo katika Kata Yombo.

**UJENZI WA KITUO CHA AFYA MATIMBWA**

Ujenzi wa kituo cha Afya Matimbwa umelenga kuboresha huduma za Afya za kina, dharura na upasuaji kwa Wakina Mama wajawazito wanaopata changamoto wakati wa kujifungua (Comprehensive, emergency, Maternal and Obstetric Care – CeMOC),

ambapo huduma za upasuaji wa dharura zimesogezwa karibu na wananchi katika kupunguza vifo vya mama motto wakati wa kujifungua.

Aidha, Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Matimbwa unatarajia kuwafikia Wananchi wasiopungua **7,590** wa Kata ya Yombo na Kata jirani pamoja na wananchi kutoka Wilaya ya Kibaha Vijijini.

**UTEKELEZAJI WA MRADI.**
Mradi wa Kituo cha Afya Matimbwa ulianza rasmi tarehe **27** Julai **2018**. Kipaumbele katika utekelezaji wa mradi huu kilikuwa kujenga majengo **4** ambayo ni jengo la wazazi (maternity ward), Jengo la Upasuaji (theater), Nyumba ya Mtumishi, Jengo la Maabara na miundombinu yake.

Hadi sasa, majengo **4** pamoja na miundombinu yake ya maji, umeme pamoja na mnara wa kuvunia maji yamekamilika.
Miundombinu mingine ilihusisha mashimo **2** ya kuvunia maji na Mnara **1** wa kuweka matanki ya maji.

Hivyo katika mradi huu jumla ya majengo **4** yamekamilika kwa asimilia 100 na miundombinu mingine iliyopangwa.

**GHARAMA ZA MRADI**
Mradi huu hadi sasa umegharimu kiasi cha **Tshs. 432,887,750.00** ambapo, Tsh. **400,000,000** ni fedha iliyopokelewa kutoka **OR – TAMISEMI** na **Tshs. 32,887,750** ni mchango wa Halmashauri, nguvu za wananchi na wadau.
Mradi huu umetekelezwa kwa njia ya ***"Force Account"*** kama ilivyoagizwa na **OR – TAMISEMI.**





**Jengo la Upasuaji lililounganishwa na Jengo la wodi ya wazazi**





***Nyumba ya Mtumishi*** ***Jengo la Maabara***

**MAFANIKIO YA MRADI**

Wananchi takribani 7590 wa Kata ya Yombo kwa kipindi cha awamu nne zilizopita hawakuwahi kuwa na kituo cha Afya, hivyo ili kupata matibabu ya uhakika iliwalazimu kusafiri umbali wa kilomita 30 kufuata huduma za Afya katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo.

Hivyo, utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa kituo cha Afya Matimbwa umekuwa ni mkombozi wa Wananchi wa Kata ya Yombo yenye Vijiji **4** na Vitongoji **31** Kwani sasa wanaweza kupata huduma za uhakika za Afya katika Kituo kipya cha Afya Matimbwa ndani ya Kata yao ya Yombo.

Mradi huu utaipandisha hadhi Zahanati ya Matimbwa kuwa Kituo cha Afya Matimbwa.

Kituo hiki kipya cha Afya Matimbwa bado hakijaanza kufanya kazi rasmi kwani kinasubiri kupokea vifaa tiba kutoka MSD, na kitaanza kazi rasmi mara tu baada ya kupokea vifaa tiba hivyo.

**UBORESHAJI UTOAJI HUDUMA KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA BAGAMOYO**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Maendeleo ya Sekta ya Afya imeboresha hali ya utoaji huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kujenga na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za Afya.

Taasisi ya Dhi – Nureyin kutoka Saudi Arabia, ambayo kwa hapa Tanzania makao yake makuu yapo Mkoani Iringa, imefadhili ujenzi wa jengo la kupokelea wagonjwa wa dharura na wodi mpya ya wazazi pamoja na kutoa vifaa tiba vyote katika majengo hayo mapya mawili ambayo tayari yameanza kutoa huduma kwa Wanachi wa Bagamoyo.

**MAJENGO YALIYOJENGWA KWA UFADHILI WA TAASISI YA DHI - NUREYIN**



***Jengo la huduma za dharura***



***Wodi mpya ya wazazi***

## UANZISHWAJI WA DUKA LA DAWA LA JAMII KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA BAGAMOYO

Hali kadhalika, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo pia imetekeleza ujenzi wa duka jipya la dawa la jamii linalohudumia wagonjwa wanaotumia bima za Afya kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na mfuko wa Afya ya jamii ulioboreshwa yaani CHF iliyoboreshwa.
Pia wagonjwa wasiotumia bima za Afya wanapata huduma ya dawa katika duka hilo kwa bei nafuu zaidi hivyo kuwapunguzia kadhia ya kwenda kununua dawa katika maduka mengine ya dawa ambayo mara nyingi hulalamikiwa na Wananchi kuuza dawa kwa bei ya juu.

Duka hili jipya la dawa limekuwa msaada mkubwa kwa Wananchi kwani limeongeza upatikanaji wa dawa wa uhakika kwa wagonjwa, pia limeongeza msukumo wa Wananchi kujiunga na huduma za Bima ya Afya za NHIF na CHF iliyoboreshwa zilizo nafuu na ambazo Wananchi wa hali ya chini wanaweza kuzimudu, hivyo kujihakikishia kupata huduma za Afya pale wanapozihitaji.




***Duka la dawa za Jamii katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo***

**MIRADI MINGINEYO YA SEKTA AFYA ILIYOTEKELEZWA**

Katika kipindi cha Miaka minne ya Uongozi wa Mhe. Rais John Pombe Joseph Magufuli, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo pia imefanikiwa kuboresha miundombinu ya Sekta ya Afya, kwa kutekeleza Ujenzi wa miradi mingine kama, Ujenzi wa Zahanati

mpya ya Kimalang'ombe iliyopo katika Kata ya Nia Njema, Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi katika Zahanati ya Kaole, Ujenzi wa Wodi ya wazazi katika Zahanati ya Mapinga na Uboreshaji pamoja na uanzishwaji wa huduma kwa mara ya kwanza katika Zahanati ya Kitame iliyopo katika Kata ya Makurunge na Zahanati ya Buma iliyopo katika Kata ya Kiromo.

Miradi hii yote imetekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo na Wananchi wa maeneo husika.





***Jengo la Zahanati ya Buma*** ***Jengo la Zahanati ya Kitame***





***Nyumba ya Mtumishi Zahanati ya Buma; Nyumba ya Mtumishi Zahanati ya Kaole***

**HUDUMA ZA AFYA KUANZA KUTOLEWA KATIKA ZAHANATI YA KITAME**

Eneo la Kitame, lipo katika Kata ya Makurunge takribani km 51 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Kitongoji hiki cha Kitame ni moja ya Vitongoji vilivyo mbali na makao makuu ya Halamshauri, lakini pia kina chan gamoto kubwa ya miundo mbinu ya usafiri hasa kipindi cha mvua.

Kitongoji cha Kitame chenye Wakazi takribani 560 katika kipindi cha miaka 4 iliyopita hakikuwahi kuwa na kituo cha kutolea huduma za Afya, hivyo kuwalazimu wananchi wa Kitongoji hiki kufuata huduma makao makuu ya Kata katika zahanati ya

Makurunge au katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, hivyo kutumia gharama kubwa kufuata huduma za Afya hasa huduma muhimu za Afya ya mama na mtoto, na si gharama tu bali pia hali hii ilipelekea vifo ambayo vingeweza kuzuilika vya wakina mama wakati wa kujifungua na watoto walio chini ya miaka mitano, kwa kuchelewa kupata huduma za matibabu mapema.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana na Idara ya Afya imehakikisha imekamilisha ujenzi wa Zahanati ya Kitame na kupeleka mganga na mhudumu wa Afya katika Zahanati hiyo.

Wananchi wa Kitongoji cha Kitame kwa mara ya kwanza wameanza kupata huduma za Afya katika Kitongoji chao na kuondokana na changamoto ya kufuata huduma za Afya mbali na makazi yao, na kituo hiki ni ukombozi wa Wananchi hawa waliohitaji sana huduma hizi, hasusani wakina mama na watoto.

**UJENZI WA ZAHANATI MPYA YA KIMALANG'OMBE**





***Zahanati Mpya ya Kimalang'ombe ikiwa katika hatua za ukamilishaji wake. Ujenzi wa Zahanati hii hadi sasa umegharimu jumla ya Tshs. 25,993,500/- fedha kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri, nguvu za Wananchi na michango ya wadau. Mradi huu utahitaji jumla ya Tshs. 157,000,000/- ili ukamilike na uanze kuhudumia wananchi.***

**UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA KUSUBIRIA HUDUMA**

Baada ya kuona usumbufu mkubwa ambao Wagonjwa ama ndugu wa wagonjwa wanaupata kwa kukosa mahali maalum pa kukaa kusubiri wanapofika Hospitali ya Wilaya kupata huduma, Halmashauri ili kutatua changamoto hiyo imeweza kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la kupumzikia wagonjwa wakati wakisubiri kupatiwa huduma ya matibabu, lakini jengo hili pia hutumika na ndugu wa wagonjwa wanapokuwa wanasubiri muda wa kuingia wodini kuona wagonjwa wao waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo.

Mradi huu umetekelezwa kwa gharama ya **Tshs. 20,000,000** fedha za matengenezo kutoka mfuko wa Taifa wa Afya ya jamii (NHIF).



***Jengo linalotumika na wateja kusubiria huduma Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo***

**SEKTA YA ELIMU**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tunajivunia utoaji wa huduma bora za elimu Msingi na Sekondari kwani kwa miaka mitatu mfululizo, Halmashauri imefanikiwa kufaulisha vizuri wanafunzi wa darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita na kushika nafasi za juu kitaifa.

**ELIMU MSINGI**

Sekta hii pamoja na mambo mengine, ina jukumu kubwa la kusimamia uendeshaji wa Elimu ya Awali, Msingi, Ufundi Stadi na Elimu ya Watu Wazima.

Ufanisi katika sekta ya elimu Msingi kwa kiasi kikubwa unategemea upatikanaji wa Takwimu Sahihi za wanafunzi, Walimu, Miundombinu na Viashiria vya elimu. Upatikanaji wa Takwimu sahihi umeiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kupiga hatua kubwa za maendeleo ikiwa ni pamoja na;

i) Kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa na kuhitimu darasa la VII, hili likienda sambamba na uongezaji wa vyumba vya madarasa pamoja na miundombinu yake.

ii) Kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa watoto itakayowawezesha kufaulu elimu ya msingi kwa asilimia **(100%)** kisha kujiunga na elimu ya Sekondari.

**IDADI YA SHULE ZA MSINGI ZILIZOPO, WANAFUNZI NA WALIMU.**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ina jumla ya shule za Msingi **51** kati ya shule hizo **34** ni za Serikali na Shule **17** binafsi na taasisi za dini.

Shule za Serikali zina jumla ya wanafunzi **29027** wakiwemo wavulana **14441** na wasichana **14586.** Pia shule za Serikali zina jumla ya Walimu **680** wakiwemo wanaume **180** na wanawake **500.**

**IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA NA MATUNDU YA VYOO**

| AINA | HITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| MADARASA | 734 | 420 | 314 |
| VYOO -WALIMU | 128 | 87 | 41 |
| VYOO - WAV | 627 | 296 | 331 |
| VYOO - WAS | 724 | 318 | 406 |

**MAFANIKIO**

Mojawapo ya vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na **Mhe. Rais; Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** katika Sekta ya elimu Msingi ni kuboresha miundombinu inayotetekelezwa na fedha za Rukuzu ya Miradi ya maendeleo kutoka Serikali kuu (**EP4R),** na fedha kutoka vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na kutoa elimu ya Msingi kwa fedha za Ruzuku ya uendeshaji **(Elimu Bila Malipo).**

Katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya awamu ya tano, yaani kuanzia **2016/2017** hadi **2018/2019,** Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeweza kupokea na kutumia jumla ya **Tshs. 1,035,806,735.00/-** fedha ambazo zilielekezwa kuboresha Sekta ya Elimu Msingi na miundombinu yake.

**A: Jedwali likionesha mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs. 1,035,806,735.00/- katika kipindi cha Mwaka 2016/17 – 2018/2019**

| **MAPATO YA NDANI 2016/017 – 2019/020** | | |
|---|---|---|
| **MWAKA** | **KIASI** | **MRADI** |
| 2016017 | 28,998,882 | Kwa ajili ya ujenzi wa vyoo katika S/Msingi 9 |
| 2017/018 | 0 | |
| 2018/019 | 15,000,000 | Kujenga matundu 10 ya vyoo S/Kiharaka na darasa 1 S/Msingi Mtoni |
| **Jumla ndogo** | **43,998,882** | |
| | | |
| **ELIMU BILA MALIPO** | | |
| **2016/017** | 0 | |
| **2017/018** | 255,872,885 | Ruzuku ya uendeshaji |
| **2018/019** | 301,127,997 | Ruzuku ya uendeshaji |
| **Jumla ndogo** | **557,000.882** | |
| | | |
| **EP4R 2016/017 – 2019/020** | | |
| **2016/017** | 1,423,948 | Ujenzi wa matundu S/Msingi mwavi |
| | 19,519,956.79 | Ujenzi wa vyumba 7 vya madarasa katika shule za misingi |
| **2017/018** | 163,873,066 | Kujenga vyumba vya madara 16 vya madarasa, matundu 12 ya vyoo na ofisi 1 |
| **2018/019** | 250,000,000 | Kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 21 |
| **Jumla EP4R** | **434,816,971** | |
| **MAPATO YA NDANI + EP4R** | **1,035,806,735** | |

Halikadhalika, utoaji wa elimu bila malipo kumeongeza chachu na mwamko kwa wazazi kuwaandikisha watoto wote waliofikia umri wa kuanza darasa la kwanza, lakini wanafunzi walioko shuleni pia kupitia fedha za EP4R Serikali imeweza kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa kujenga vyumba vya madarasa pamoja na madawati. Jitihada hizi zote, kwa pamoja zimeongeza kiwango cha ufaulu pamoja na watoto wanaochaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza.

**B: Jedwali kuonyesha wanafunzi walioandikishwa elimu ya awali 2017-2019**

| **Mwaka.** | **Maoteo** | | | **walioandikishwa** | | | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **WAV** | **WAS** | **JML** | **WAV** | **WAS** | **JML** | |
| 2017 | 1734 | 1802 | 3536 | 1345 | 1369 | 2714 | 77 |
| 2018 | 2329 | 2315 | 4644 | 1390 | 1377 | 2767 | 60 |
| 2019 | 2473 | 2230 | 4703 | 1588 | 1462 | 3047 | 65 |

**C: Jedwali kuonesha wanafunzi walioandikishwa Darasa la kwanza 2017 - 2019**

| **Mwaka.** | **Maoteo** | | | **walioandikishwa** | | | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **WAV** | **WAS** | **JML** | **WAV** | **WAS** | **JML** | |
| **2017** | 1881 | 1929 | **3810** | 2046 | 1971 | **4017** | **105** |
| **2018** | 1960 | 1933 | **3893** | 2144 | 2167 | **4311** | **111** |
| **2019** | 2309 | 2018 | **4327** | 2396 | 2250 | **4646** | **112** |

**D: Jedwali kuonesha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kwa jumla darasa la I – VII 2017 – 2019**

| **MWAKA** | **WAVULANA** | **WASICHANA** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| **2017** | 13836 | 13537 | **27373** |
| **2018** | 12356 | 11720 | **24076** |
| **2019** | 14441 | 14586 | **29027** |

Aidha, jitihada za kuboresha na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa, pamoja na miundombinu yake, kumechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufaulu wa wanafunzi wanaomaliza elimu ya darasa la saba kama inavyoonekana kweye jedwali hapa chini.

**UFAULU**

| **MWAKA** | **walioandikishwa** | | | **Waliofanya mtihani** | | | **%** | **waliofaulu** | | | **Nafasi.** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **WAV** | **WAS** | **JML** | **WAV** | **WAS** | **JML** | | **WAV** | **WAS** | **JML** | **MKOA** | **TAIFA** |
| **2016** | 898 | 1078 | **1976** | 703 | 841 | **1544** | 78 | 703 | 841 | 1544 | **2** | |
| **2017** | 1139 | 1209 | **2348** | 925 | 951 | **1876** | 80 | 925 | 951 | 1876 | **2** | **51** |
| **2018** | 1322 | 1356 | **2679** | 1168 | 1195 | **2363** | 88 | 1168 | 1195 | 2363 | **3** | **29** |
| **2019** | 1249 | 1326 | **2575** | | | | | | | | | |

**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA NA SEKTA YA ELIMU MSINGI KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2016-2019.**

## I. SHULE YA MSINGI UKUNI – KATA YA DUNDA




***Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa na matundu 06 ya vyoo, katika shule ya msingi ukuni – Kata ya Dunda***

***Mradi umegharimu shilingi milioni 66,600,000.00/-, fedha za EP4R***

## II. SHULE MPYA YA MSINGI MSHIKAMANO – KATA YA ZINGA






***Ujenzi wa vyumba 9 vya madarasa na matundu 16 ya vyoo katika Shule ya Msingi Mshikamano – Zinga.***
***Utekelezaji wa Mradi umegharimu tshs. 149,000,000.00/- kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.***

III. SHULE MPYA YA MSINGI KIMERE – KATA YA MAPINGA





***Ujenzi wa Vyumba 03 vya madarasa na matundu 06 ya vyoo katika Shule mpya ya Msingi Kimere***
***Utekelezaji wa mradi umegharimu jumla ya TSHS. 66,600,000.00/- Fedha za (EP4R) na***
***nguvu za Wananchi ni 6,681,000/-***

IV. SHULE MPYA YA MSINGI KITOPENI





**Ujenzi umegharimu Kiasi cha Shilingi 10,000,000/-**
**Mradi huu umetekelezwa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri, Wananchi na Michango ya wadau wa maendeleo.**

**UJENZI WA VYUMBA VITATU VYA MADARASA KATIKA SHULE YA MSINGI MTAKUJA – KATA YA FUKAYOSI**

Idara ya elimu Msingi pia imetekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Mtakuja, iliyopo katika Kata ya Fukayosi.

Shule hii yenye jumla ya Wanafunzi ilikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa ambapo Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imetekeleza ujenzi wa vyumva vitatu vya madarasa ambavyo tayari vimeanza kutumika na kumaliza changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa katika Shule hiyo.

Mradi huu umegharimu jumla ya **Tshs. 36,688,066/-** Hadi kukamilika kwake.





**MRADI WA KUONGEZA VYUMBA 03 VYA MADARASA KATIKA SHULE YA MSINGI MAPINGA**

Shule ya Msingi Mapinga imekuwa na ongezeko kubwa la Wanafunzi kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita hivyo kupelekea Halmashauri na Wananchi wa Vitongoji vya Kata ya Kerege kuamua kuanza mradi wa Ujenzi wa vyumba Vinne vya Madarasa katika Shule hii kongwe ya Msingi ili kuondokana na kero ya msongamano wa wanafunzi madarasani na kutengeneza mazingira rafiki ya kufundisha kwa Walimu na kusoma kwa Wanafunzi Shuleni hapo.
Utekelezaji wa mradi huu umegharimu jumla ya **Tshs. 20,000,000/-** zilizotumika katika ukamilishaji toka Halmashaauri baada ya Wanaachi kutekelekeza mradi huo hadi kufikia hatua ya lenta.





***Vyumba 04 vya madarasa katika Shule ya Msingi Mapinga***

**SEKTA YA ELIMU SEKONDARI**
Sekta ya Elimu Sekondari, katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2016/2017 hadi 2018/2019 imefanikiwa kupiga hatua kubwa ya utekelezaji wa kuboresha miundombinu ambayo imeinua kiwango cha elimu ya Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Aidha, Halmashauri ya Bagamoyo ina jumla ya Shule za Sekondari **21** zikiwemo Shule za Serikali **09** na za watu binafsi/Taasisi **12** ambapo, Halmashauri ina jumla ya wanafunzi **10,716** kati yao waliopo katika Shule za Serikali ni **5,006** (Wavulana **2,483**

na Wasichana **2,523)** na Shule za binafsi/Taasisi ni Wanafunzi **5,710 (**Wavulana **2,591 na** Wasichana **3,119).**
Idadi ya Walimu katika Shule za Serikali ni **463** ambapo waalimu wa masomo ya Sayansi n**i 78** na wa masomo ya Sanaa **385.** Hata hivyo, bado Halmashauri ina upungufu wa walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati **61.**

**MAFANIKIO**

Katika kipindi cha miaka 4, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imefanikiwa kuboresha kiwango cha utoaji huduma za elimu Sekondari kwa kuboresha miundo mbinu ya madarasa, nyumba za walimu, maabara, maktaba, pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**Jedwali kuonesha idadi ya madarasa, maktaba, maabara, matundu ya vyoo na madawati**

| AINA | HITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| MADARASA | 192 | 124 | 68 |
| MAKTABA | 9 | 2 | 8 |
| MAABARA | 27 | 8 | 19 |
| VYOO | 308 | 154 | 154 |
| MADAWATI | 7697 | 4152 | 3545 |

**SHULE ZA SEKONDARI ZA KATA**
Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ina jumla ya Kata 11, Halmashauri imefanikiwa kujenga Shule za Sekondari za Kata katika Kata 08. Kati ya Shule hizi 08 za Sekondari za Kata, Shule mbili zimejengwa katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya awamu ya tano.

Uwepo wa Shule za Sekondari za Kata katika Halmashauri umerahisisha utoaji wa huduma ya elimu ya Sekondari kwa Wananchi wa Bagamoyo hususani wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza kila Mwaka.

Halikadhalika, uwepo wa Shule za Sekondari za Kata umeongeza fursa ya kupata elimu kwa Wanafunzi wa Bagamoyo ambao, hapo awali wengi walikosa fursa ya kuendelea na elimu ya Sekondari mara walipomaliza elimu ya Msingi, kwani Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilikuwa na Shule moja tu ya Sekondari ya Serikali ambayo ni Shule kongwe ya Sekondari Bagamoyo.

**MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA SEKTA YA ELIMU SEKONDARI**
Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo katika kipindi cha mwaka 2016/017 hadi 2018/019 imeendelea kufanya vizuri katika sekta ya elimu kwa utoaji wa huduma bora za elimu. Katika kufanikisha adhima ya Mhe. Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha kila mtanzania anapata elimu bora, Halmashauri imeweza kupokea na kutumia jumla fedha za kitanzia **Tshs. 1,303,519,784.67/-** kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu Sekondari, fedha hizi ni pamoja na fedha za mapato ya ndani, fedha za Elimu Bila Malipo na fedha za EP4R

**Jedwali likionesha mapokezi ya fedha za utekelezaji miradi ya maendeleo za mapato ya ndani, Elimu Bila Malipo na EP4R.**

| | | |
|---|---|---|
| **MAPATO YA NDANI 2016/017 – 2019/020** | | |
| **MWAKA** | **KIASI** | **MRADI** |
| 2016017 | 0 | |
| 2017/018 | 5,000,000 | Kutengeneza fanicha S.S Kerege |
| 2018/019 | 5,000,000 | Kutengeneza fanicha S.S. Kiromo |
| **Jumla ndogo** | **10,000,000** | |
| **ELIMU BURE** | | |
| **2016/017** | 0 | |
| **2017/018** | 535,583,880 | Ruzuku ya uendeshaji |
| **2018/019** | 596,036,352 | Ruzuku ya uendeshaji |
| **Jumla ndogo** | **1,131,620,232** | |
| | | |
| **EP4R 2016/017 – 2019/020** | | |
| **2016** | 9,616,887.67 | Kukarabati sakafu vymba 6 vya madarasa na ofis 1 katika Shule ya Sekondari Hassanari Damj. |
| | 1,600,000.00 | Ununuzi wa Stul za Maabara Shule ya Sekondari Fukayosi |
| | 3,500,000.00 | Kukarabati vyoo Shule ya Sekondari Dunda |
| | 6,000,000.00 | Kujenga vyoo Bagamoyo Sekondari |
| **Jumla ndogo** | **20,716,887.67** | |
| **2017** | 2,000,000.0 | Kuggharamia miundombinu ya kuksanyia takwimu Idarani |
| | 46,009,599.00 | Kukamilisha vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Kingani |
| | 30,673,066.00 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Sekondari Mapinga |
| **Jumla ndogo** | **78,682,665.00** | |
| **2018** | 37,500,000.00 | Kukamilisha vyumba 3 vya madarasa Shule ya Sekondari Mapinga |
| | 25,000,000.00 | Kukamilisha vyumba 2 vya maabara Shule ya Sekondari Kingani |
| **Jumla ndogo** | **62,500,000.00** | |
| **Jumla EP4R** | **161,899,522.67** | |
| **MAPATO YA NDANI + EP4R** | **1,303,519,784.67** | |

Utekelezaji wa miradi ya EP4R imekuwa chachu kubwa ya kuongeza ufanisi katika utoaji huduma za elimu ya Sekondari katika Halmashauri kwa kuboresha mazingira ya kutoa elimu baada ya kuongezeka kwa miundombinu ya madarasa, maabara na nyumba za walimu.

**ELIMU BILA MALIPO**

Utekelezaji wa Sera ya Serikali ya elimu bila malipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imekuwa yenye mafanikio makubwa kwa ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza, lakini kuondoa utoro kwa wanafunzi Shuleni.

Hulka ya wakazi wa maeneo ya Pwani, hasa mwambao huu wa Bagamoyo, wengi wao hawana mwamko wa kupeleka watoto Shule kupata elimu hasa elimu ya Sekondari kwa kuwa wanakuwa wamefikia umri wa kubalehe, hivyo wazazi wengi wa ukanda huu hupendelea kuwafanyia mila watoto wao hasa wa Kike kwa kuwacheza ngoma na kisha kuwaozesha katika umri mdogo ambao ungestahili wao kuwa Shuleni wakiendelea kupata elimu ya Sekondari.

**UJENZI WA MAABARA**

Ili kuendana na Sera ya Serikali ya awamu ya tano ya Tanzania ya Viwanda, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inashiriki kuandaa wataalamu wengi wa Sayansi kwa kuhakikisha inajenga maabara katika Shule za Sekondari, zitakazowajengea uwezo Wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi kwani maabara hizi zinajenga msingi wa ubobezi katika fani ya Sayansi, ili Wanafunzi hao waje kushiriki katika kuijenga Tanzania ya Viwanda.

Jumla ya maabara 02 zimejengwa katika kipindi cha miaka 04 ya uongozi wa Serikali ya awamu ya tano. Maabara hizi zimejengwa katika Shule ya Sekondari Kingani na Shule ya Sekondari Fukayosi.





***Vyumba 02 vya Maabara uliogharimu Tshs. 46, 009,599.51/- katika Shule ya Sekondari Kingani.***

**UFAULU**

Katika kipindi cha cha mwaka 2016 hadi 2018, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imekuw na mwendelezo chanya wa ufauru wa mitihani ya Taifa kwa kidado cha pili, nne na sita. Matokeo haya yametokana na uboreshaji wa miundombinu katika Shule zote kwa kadri bajeti inavyoruhusu. Matokea haya pia yamekuwa na mchango mkubwa katika kupandisha nafasi ya Mkoa Kitaifa.

**MIKAKATI YA KUBORESHA UFAULU**

Idara ya Elimu Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imejiwekea mikakati kadha wa kadha ya kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi katika Shule za Sekondari kwenye Halmashauri ni wa uhakika.

Baadhi ya mikakati hii ni pamoja na vikao vya wadau wa elimu ngazi ya Wilaya, ambapo wadau hawa wa elimu kutoka katika Shule binafsi na Shule za Serikali hukutana katika vikao maalum kujadili mbinu mbalimbali za kuboresha elimu katika Halmashauri. Katika kipindi cha Mwaka 2016 – 2019 jumla ya vikao … vimefanyika.

Vikao hivi hufanyika mara moja kila mwezi, na hutumika pia kubadilishana uzoefu kati ya walimu juu ya namna ya kuboresha mbinu za ufundishaji wanafunzi.

Mkakati mwingine ni kufanya kikao cha tathmini ya mwenendo wa utoaji huduma za elimu ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Katika kikao hiki, wadau mbalimbali wa elimu ndani ya Halmashauri hujadili kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka husika, changamoto zilizojitokeza zinazoweza kushusha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi na namna ya kukabiliana nazo. Kikao hiki cha tathmini ya elimu hufanyika mara moja kila Mwaka.

Mkakati mwingine unaotekelezwa ni kikao kazi maalum kati ya Wakuu wa Shule za Sekondari katika Halmashauri. Kikao kazi hiki hufanyika mara moja kila Mwaka kwa wakuu wa Shule za Sekondari binafsi na za Serikali, kikiwa na lengo la kuwanoa wakuu wa Shule juu ya mipango mahsusi ya Halmashauri ya kuboresha elimu, mbinu za kuboresha elimu ya Sekondari ambazo hufundishwa katika kikao hiko, ambapo wakuu hao wa Shule hutakiwa kwenda kuzirithisha kwa walimu walio chini yao katika Shule wanazozisimamia.

Mkakati wa tusome pamoja, Idara ya elimu imebuni utaratibu maalum wa walimu kuwasaidia wanafunzi mmoja mmoja, utaratibu uitwao ***"tusome pamoja"*** katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. ambapo mwalimu hukaa na mwanafunzi mmoja mmoja na kumsaidia mada ambayo imemtatiza mwanafunzi ili kumjengea uelewa zaidi mwanafunzi huyo wa kuelewa kila mada zinazofundishwa darasani. Utaratibu huu ni msaada mkubwa kwa wanafunzi kwani umeonesha mafanikio makubwa kwa kuongezeka kwa uelewa wa masomo kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari

**Jedwali likionyesha nafasi ya Ufaulu wa Halmashauri Kimkoa na Kitaifa.**

| | **KIDATO CHA PILI** | | | **KIDATO CHA NNE** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA.** | **IDADI.** | **NAFASI KIMKOA** | **KITAIFA.** | **IDADI** | **NAFASI KIMKOA** | **KITAIFA.** |
| **2018** | 2,312 | 1 | 1 | 1,782 | 1 | 1 |
| **2017** | 2,074 | 1 | 3 | 1,667 | 1 | 1 |
| **2016** | 1986 | 1 | 17 | 1,583 | 3 | 35 |

**UFUATILIAJI WA MASUALA YA ELIMU KATIKA WILAYA**

Halmashauri ina wataalam wa elimu katika kila Kata ambao ni Maafisa elimu Kata wenye jukumu la kufuatilia shughuli za elimu katika Kata husika, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na utoro wa walimu na wanafunzi mashuleni, kutatua changamoto mbalimbali za kielimu pia kusimamia miradi ya maendeleo ya Sekta ya elimu inayotekelezwa katika Kata husika.

Wizara ya elimu na mafunzo ya Ufundi katika kuhakikisha ufuatiliaji huu wa shughuli za elimu katika Halmashauri unakuwa wenye tija, imetoa jumla ya pikipiki 11 kwa waratibu elimu Kata 11 wa Kata 11 za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambazo zimerahisisha suala la ufuatiliaji na zimechochea kwa kiasi kikubwa ari ya waratibu

elimu Kata katika kufuatilia na kusimamia shughuli za elimu katika Kata wanazosimamia.




**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE**

### I. SHULE YA SEKONDARI FUKAYOSI.

Shule ya sekondari Fukayosi ipo katika Kata ya fukayosi, Shule hii ilijengwa kwa ufadhili wa taasisi isiyo ya Serikali ya ***Good neighbors*** kwa ushirikiano na kampuni ya Kijapan ya KIA chini ya mradi wao wa Green Light.

Utekelezaji wa mradi huu ulihusisha ujenzi wa vyumba 08 vya madarasa, Ofisi 01 ya Walimu, Vyumba 02 vya maabara, Chumba 01 cha kompyuta, Matundu 12 ya vyoo, na nyumba 01 ya mwalimu. Utekelezaji wa mradi huu uligharimu jumla ya **Tshs. Bil 1.2**





***Jengo la vyumba vinne vya madarasa; Sekondari*** ***Nyumba ya Mtumishi Fukayosi***

### II. SHULE MPYA YA SEKONDARI MAPINGA - KATA YA MAPINGA





Kata ya Mapinga ni moja ya Kata ambazo hazikuwahi kuwa na Shule ya Serikali ya Sekondari, hivyo kwa mara ya kwanza Wananchi wa Kata hii watanufaika na huduma ya elimu ya Sekondari baada ya utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Mapinga.

Ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa katika shule Mpya ya sekondari Mapinga, na Ofisi 01 ya Walimu iliyojengwa na mdau wa maendeleo Hill group of companies.

Utekelezaji wa mradi huu umegharimu jumla ya Tshs. 68,173,066.00 Fedha toka ruzuku ya miradi ya maendeleo sekta ya Elimu, EP4R katika Mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019.

**UKARABATI WA MAJENGO YA SHULE YA SEKONDARI BAGAMOYO**





***Bweni la wavulana la madaraka kabla na baada ya ukarabati***





*Bweni la wavulana la Mwenge kabla na baada ya ukarabati*









*Mabweni mawili ya wasichana kabla na baada ya ukarabati*





***Jengo la utawala / Ofisi ya Walimu kabla na baada ya ukarabati***





***Nyumba za walimu*** ***Nyumba ya mwalimu Mkuu***





***Halmashauri Block, kabla na baada ya ukarabati***

***Madarasa ya wanafunzi wa kidato cha sita kabla na baada ya ukarabati***

***Jengo la maabara kabla na baada ya ukarabati***

**SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA.**

Inakadiriwa kuwa, 85% ya idadi ya watu katika Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo wanajishughulisha na kilimo ambacho ni kilimo cha kujikimu. Aidha, ni asilimia 6.7% tu ya hekta 334,632 za eneo lote la Halmashauri ya Bagamoyo ndiyo linatumika kwa kilimo, kwa mazao yote ya biashara na chakula ambayo ni pamoja na mahindi, mpunga, mihogo, viazi vitamu, korosho, mananasi, machungwa, maembe na alizeti.
Hivyo, kupitia Sekta ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika, Halmashauri ya Bagamoyo katika kipindi cha miaka minne **(2016/2017 hadi 2019/2020)** imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali za Maendeleo ya Kilimo ikiwemo Miradi ya Kilimo.

Miongoni mwa Mafanikio yaliyopatikana kupitia shughuli za kilimo katika kipindi cha miaka minne ni kama ifuatavyo:

I. **Uzalishaji wa zao la mpunga katika Skimu ya Umwagiliaji ya Bagamoyo (BIDP):**

Katika kipindi cha miaka minne **(2016/2017 hadi 2019/2020)** Skimu ya Umwagiliaji ya Bagamoyo yenye eneo lenye ukubwa wa **Hekta 57.5,** hutumika kuzalisha zao la mpunga katika misimu miwili ya Vuli na Masika kila mwaka na hivyo, kuzalisha wastani wa **Tani 3.7** za mpunga kwa mwaka. Mavuno haya yamesaidia kuongeza uhakika wa chakula na kipato kwa wakulima.

### II. Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji Skimu ya BIDP

Shughuli za Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika Skimu ya BIDP zimegharimu kiasi cha **Tshs. 233,685,814/=** kati ya **Tshs. 294,000,000/=** zilizoidhinishwa.

Ukarabati huu umesaidia kupunguza upotevu wa maji ya kumwagilia kutoka **75% - 50%.** Pia umesaidia kufikisha maji kwenye mashamba kwa kiwango kinachokubalika katika msimu wa kilimo kutoka **30% - 60%.**



***Miundombinu ya mifereji ya maji katika skimu ya umwagiliaji ya Tegemeo (BIDP)***

### III. Mashine ya kuvunia mpunga (Combine Harvester)

Uwepo wa mashine ya kuvunia mpunga (Combine Harvester) kumerahisisha uvunaji na kupunguza upotevu wa mavuno.

### IV. Ghala la kuhifadhia mpunga

Uwepo wa ghala la kuhifadhia mpunga kumesaidia wakulima kuhifadhi kiasi cha **60%** ya mavuno kwa kulipa **shilingi 20/=** kwa kila kilo moja ya mpunga anayohifadhi baada ya kuvuna na **40%** anaachiwa kwenda nao nyumbani kama chakula.



***MRADI WA SKIMU YA UMWAGILIAJI TEGEMEO (BIDP) – KATA YA MAGOMENI***

### V. MASHAMBA DARASA.

Ili kuwasaidia Wananchi wa Bagamoyo kulima kilimo chenye tija, kitakachowasaidia kuboresha lishe na kuwakwamua kiuchumi, Halmashauri kupitia Idara ya Kilimo, imeanzisha mashamba darasa **03** Katika Kata za Yombo na Kiromo, Mashamba darasa haya yameleta tija kubwa kwa Wakulima kwani yamewasaidia kupata elimu ya kulima kisasa, kwa ubora na kibiashara hivyo kuwakwamua kiuchumi.

Mashamba darasa haya 03, yana ukubwa wa ekari 01 kila moja, na yameanzishwa maalum kwa ajili ya kutoa elimu ya kilimo cha kunde, mihogo na viazi lishe.

Katika kipindi cha Mwaka 2018/2019 Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 3,538,000/=,** kuwezesha kikundi cha wakulima katika Kata ya Kiromo kuzalisha zao la kunde, Vikundi viwili toka Kata ya Yombo ambavyo ni kikundi cha wakulima wa kijiji cha Kongo walizalisha viazi lishe na kikundi cha wakulima kutoka Kijiji cha Chasimba walizalisha mhogo bora.

Lengo kuu la mashamba darasa haya ni kutoa elimu juu ya kuzalisha mazao yenye virutubisho vya lishe na yenye faida kibiashara, yakiwemo mazao ya kunde na viazi lishe na mhogo. Aina za mbegu zilizotumika ni Vuli 1 na 2 kwa upande wa kunde, Viazi Lishe ni Kabode, ujumla, Mataya na Jewele na kwa upande wa mhogo wakulima walielekezwa kutumia mbegu za mkuranga one na kiroba.



***Shamba darasa la mihogo - Chasimba***



***Kunde zilizooteshwa katika shamba darasa Kiromo***

Aidha wakulima walitumia fursa hii kuwafundisha wakulima wengine juu ya umuhimu wa kutumia viazi lishe kama chakula kutokana na kuwa na vitamin ‘A’ kwa wingi. Wakulima pia kwa kutumia viazi lishe waliweza kujifunza jinsi ya kusindika bidhaa mbalimbali kama vile unga, maandazi, chapati na uji ambao waliuuza kwa wateja wengine



***Viazi lishe vikiwa tayari kuvunwa katika shamba darasa la Viazi lishe Kongo.***

## VI. Uzalishaji wa mbegu bora za muhogo daraja la Kuazimiwa Ubora (QDS)

Katika kipindi cha miaka mitatu **(2016/2017 hadi 2018/2019),** Halmashauri kwa kushirikiana na Kampuni ya Centre for Agriculture and Bioscience International (CABI) imefanikiwa kuanzisha Ekari 10 za mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora za muhogo daraja la Kuazimiwa Ubora (QDS) katika vijiji vya Yombo na Mwavi kupitia vikundi vya Kituruma katika Kata ya Yombo, Kirohosafi na Tushikamane vyote vya Mwavi katika Kata ya Fukayosi. Mashamba haya yanatarajiwa kuzalisha **pingili 1,004,800/=** za vipando vya muhogo ambavyo vinatosha kupanda jumla ya **Ekari 251.2** za mashamba ya muhogo.

Kikundi cha Kituruma kutoka Kata ya Yombo, kupitia mradi huu, kimefanikiwa kujenga jengo lenye mashine ya kusaga unga wa mhogo ambao hufungashwa katika mifuko maalumu ya kisasa ya kilo 1 na kilo 5 na kuuza ndani na nje ya Mji wa Bagamoyo, mradi huu umewasaidia wanakikundi hawa kujikwamua kiuchumi na kuboresha hali zao kimaisha.





***Mashamba ya kuzalisha mbegu za muhogo katika Kata ya Fukayosi na Yombo***

**USHIRIKA WILAYANI BAGAMOYO**

Kitengo cha Ushirika hushughulika au hufanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika **Na 6 ya mwaka 2013** pamoja na Kanuni ya vyama vya Ushirika ya **mwaka 2015**

Aidha Kitengo cha Ushirika pia hufanya kazi kwa maelekezo kupitia Waraka mbalimbali zinzotolewa na Mrajis wa vyama vya Ushirika Tanzania Bara.
Vyama vya Ushirika vilivyopo katika Halmashauri yetu ni kama vinavyoonekana hapa cfhi katika jedwali Na. 1, Amcos, SACCOS na vyama vingine vya ushirika.

Halmashauri ya Bagamoyo ina vyama vya ushirika 94. Kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 1**

| NA | AINA YA VYAMA | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | SACCOS | 57 |
| 2. | AMCOS | 5 |
| 3. | VYAMA VINGINE | 32 |
| **JUMLA** | | **94** |

**SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI**

Shughuli nyingine inayotegemewa kiuchumi na wakazi wa Bagamoyo ni ufugaji, hasa wa ng'ombe.

Mifugo inayofugwa kwa wingi ni ng'ombe, mbuzi, Kondoo, Nguruwe, Kuku na Punda.

Halmashauri ina vijiji viwili (2) vya wafugaji ambavyo ni Mkenge na Fukayosi ambapo wafugaji wengi wanakaa katika Vijiji hivyo wakitekeleza shughuli zao za ufugaji kwa ufanisi, Halmashauri imefanya hivi ili kuweka mazingira rafiki kwa wafugaji ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji, na jambo hili limeonesha tija kubwa.

**MIRADI YA SEKTA YA MIFUGO**

Sekta ya mifugo imetekeleza miradi miwili katika kipindi cha miaka minne. Miradi hii ni ujenzi na uanzishwaji wa Mnada wa mifugo Fukayosi na uboreshaji wa Machinjio, mradi unaopatikana katika Kitongoji cha Sanzale Kata ya Magomeni.

**MRADI WA UJENZI WA MNADA WA MIFUGO FUKAYOSI**

Sekta ya Mifugo katika kipindi cha miaka mitatu imetekeleza miradi ya maendeleo yenye tija na yenye kuiongezea Halmashauri kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani, baada ya Halmashauri kubuni na kutekeleza ujenzi wa mnada wa mifugo katika Kata ya Fukayosi.

Utekelezaji wa mradi huu mpaka sasa umegharimu jumla ya **Shilingi 12,000,000.00**.

Mradi huu umeanza kufanya kazi na tayari unaiingizia Halmashauri mapato hivyo kuongeza kiwango cha ukusanyaji mapato ya ndani.

**MNADA MPYA WA FUKAYOSI**

***UVUVI***

Zaidi ya 70% ya Wananachi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo wanategemea Uvuvi kama chanzo chao kikuu cha mapato ya kila siku. Pwani ya Bagamoyo ina

ukubwa wa kilomita 100 za mraba. Ina ukaribu na Kisiwa cha Unguja, na sifa za kujaa mchanga, matope, miamba ya matumbawe, majukwaa ya mwamba unaoingiliana, vitanda vya nyasi za baharini, mifereji ya maji na milango. Hii ni muhimu kwa rasilimali anuwai ya uvuvi.

Uvuvi unaofanyika ni pamoja na mitego ya vikapu, ndoano na mistari, nyavu za urefu wa 100-200 milimita na nyavu za gili. Kuna wavuvi takriban 1714 na meli 412 (utafiti wa sura ya samaki wa 2009). Bagamoyo pia ina Fursa ya Uvuvi katika Bahari Kuu

**MRADI MKAKATI WA UJENZI WA SOKO LA KISASA LA SAMAKI DUNDA**

Katika kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muunano wa Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo iliwasilisha miradi miwili ya Kimkakati ambayo ni ujenzi wa Soko la Samaki la Kisasa Kata ya Dunda na ujenzi wa stendi mpya ya mabasi Sanzale.

Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ni mojawapo kati ya Halmashauri 12 zilizopata fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa miradi ya Kimkakati, kwa Bagamoyo mradi wa Kimkakati ni ujenzi wa Soko la Samaki Dunda. Aidha, mradi huu utagharimu kiasi cha Tshs. 1.6 billioni ambapo majengo ya kipaumbele katika Soko hili ni;

- Jengo la kunadishia samaki
- Jengo la mama lishe
- Jengo la Mgahawa
- Jengo kwa ajili ya maduka an viosiki
- Choo

**MWONEKANO WA SOKO LA SAMAKI DUNDA BAADA YA KUKAMILIKA**





Mpaka sasa hatua za awali za maandalizi ya kutekeleza mradi huu zimeshafanyika ikiwa ni pamoja na kutangaza tenda na kumchagua mkandarasi wa kufanya tathmini ya athari za kimazingira (EIA) katika eneo la utekelezaji wa mradi, kumpata mhandisi mwelekezi wa mradi, halikadhalika, Halmashauri pia imeshasaini mkataba wa kuanza kwa utekelezaji wa mradi na mkandarasi mjenzi na makataba huo kuwasilishwa hazina.

Aidha, Halmashauri imeshawamisha wafanyabiashara waliokuwa katika soko la awali ili ujenzi uanze mara moja.

Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mara moja pindi Halmashauri itakapopokea fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Soko la Samaki Dunda.

**SEKTA YA UJENZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo pia katika uboreshaji wa miundo mbinu yake imetekeleza mradi wa ujenzi wa ukuta katika nyumba ya Mkurugrnzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Mradi huu uligharimu jumla ya **Tshs. Mil. 82** hadi kukamilika kwake.

**UJENZI WA UKUTA KATIKA NYUMBA YA MKURUGENZI MTENDAJI**





**SEKTA YA MAJI**

**I. MRADI WA MAJI YA BOMBA KUTOKA MTO RUVU.**

Katika kutekeleza azma ya serikali ya awamu ya tano ya kuhakikisha inawapelekea wananchi huduma ya maji safi na salama, Halmashauri ya Bagamoyo kwa kushirikiana na mamlaka ya Majisafi na Majitaka (DAWASA) imetekeleza ujenzi wa miradi mbali mbali ya huduma ya maji safi na salama katika Wilaya ya Bagamoyo.

Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na;

Ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji lenye kipenyo cha inchi **20 (DN500)** kuleta maji katika mji wa Bagamoyo lenye umbali wa **km 13** kutoka Sunguvuni (matimbwa) ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji lenye kipenyo cha inchi **16 (DN400**) kupeleka huduma ya maji safi maeneo maalum ya viwanda-Zinga (EPZ) umbali wa **km 5**, ujenzi wa mabomba ya usambazaji maji maeneo maalum ya viwanda - Zinga na maeneo ya wakazi wa Zinga kwa Awadhi, Ujenzi wa visima 10, mradi wa maji wa ujenzi wa matanki ya kuvunia maji ya Mvua katika Shule ya Sekondari Kingani, pamoja na ujenzi wa tanki la majisafi lenye ujazo wa **lita 6,000,000**.

**UJENZI WA TANKI LA MAJI UJAZO WA LITA 6,000,000 KATIKA KATA YA MAGOMENI**

Tanki hili limejengwa maalumu kwa ajili ya kusambaza maji safi katika mji wa Bagamoyo na Vitongoji vyake.

Aidha, katika kufanikisha mradi huu, utekelezaji wa Ujenzi wa tanki kwa mujibu wa mkataba ni USD **1,637,562** sawa na shilingi bilioni tatu (**Tsh 3,000,000,000**) za kitanzania. Ujenzi kwa sasa umekamilika kwa asilimia **100.**

Ni matarajio yetu kuwa kukamilika kwa mradi huu, kutawezesha kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa mji wa Bagamoyo na vitongoji vyake kutoka asilimia **66** hadi kufikia asilimia **95** ifikapo mwaka 2020.





***Ujenzi tanki la maji lenye ujazo wa lita 6,000,000 kabla na baada ya kukamilika kwake.***

**II. UJENZI WA MATANKI 9 YA KUVUNIA MAJI YA MVUA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KINGANI**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inaendelea kuunga juhudi za Serikali ya awamu ya tano kwa kutekeleza mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Taifa ya kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi nchini katika maeneo ya Pwani, mradi huu umefadhiliwa na mfuko wa Nchi masikini Duniani **(LDCF)** Least Developed Countries Fund kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais. Mradi ulianza kutekelezwa **31/7/2017** chini ya Mkandarasi Mjenzi Shamoka Building and Civil Contractors

**LENGO LA MRADI**

Lengo la mradi ni kuboresha huduma ya maji kwa wanafunzi **845,** walimu 57 pamoja na wananchi wanaoishi karibu na shule ya Sekondari kingani, kutokana na kuongezeka kwa ujazo wa bahari na kunakosababisha kuingia kwa maji ya chumvi katika maji ya ardhini (salt water intrusion) na kuathiri visima vya maji vilivyoko pembezoni mwa bahari ya Hindi.

Eneo hili la shule ya Sekondari Kingani lilipata changamoto hiyo na kusababisha maji ya visima kuwa na chumvi sana yasiyofaa tena kwa matumizi ya binadamu na mimea, hivyo kupelekea Wanafunzi hasa wa bweni katika Shule ya Sekondari Kingani pamoja

na walimu wanaoishi katika eneo la Shule hii kukosa kabisa huduma ya maji yasiyo na chumvi.

Utekelezaji wa mradi huu umekuwa ni ukombozi kwa Wanafunzi na Walimu wa Shule ya Sekondari Kingani, kwani eneo hili sasa limepata huduma ya maji ya uhakika na kurahisisha maisha yao kwa ujumla.





**Matanki 2 ya Plastiki kati ya 4 yanayotumika kuvuna maji ya mvua katika shule ya Sekondari Kingani.**







**Matanki 2 kati ya 5 ya kuvuna maji ya mvua yaliyojengwa kwa zege katika shule ya Sekondari Kingani.**

**GHARAMA ZA MRADI.**

Katika kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji shule ya Sekondari Kingani, jumla ya fedha **Tshs. 141,244,517.50** zimetumika kujenga matanki **9** yenye ujazo wa lita **35,000** (1), lita **25,000** (2), lita **15,000** (2) na lita **8000** (4) yenye jumla za ujazo wa lita **147,000.**

### III. MRADI WA UJENZI WA VISIMA 10

Katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya tano pia, Mradi wa uchimbaji wa visima 10 umetekelezwa katika Kata 05 za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambazo ni Kata ya Zinga, Kisutu, Kiromo, Magomeni na Dunda.

Shughuli zilizofanyika katika utekelezaji wa mradi huu ni kuchimba na kujenga matanki **10** ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita **15,000** kila moja na umegharimu jumla ya kiasi cha **Tshs. 688,877,958/-**



**Shule ya Msingi kidongochekundu Magomeni**



**Kisima cha maji cha Maji Coast-**



**Kisima cha maji Zinga**



**Shule ya Sekondari Dunda**

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za uwezeshaji wananchi hususani vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuwawezesha mikopo, elimu ya ujasiriamali na utaalamu ili waweze kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kujiletea maendeleo kupitia vikundi vyao vya ujasiriamali.

**DAWATI LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

Baraza la Taifa la uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) liliandaa mkakati wa mwongozo wa utekelezaji ambao ulielekeza uanzishwaji wa madawati ya Uwezeshaji na ushiriki wa Wananchi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Halmashauri.

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo katika kutekeleza maekekezo hayo ilianzisha dawati maalumu la uwezeshaji wananchi kiuchumi mnamo Mwezi Septemba 2016, dawati hili linaratibiwa na kusimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii.

Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi unafanyika katika maeneo makuu matatu ambayo ni;

a) Uwezeshaji wa mitaji; (capital)

b) Kuwajengea uwezo wa elimu ya ujasiriamali; (capacity building)

c) Kuwapa stadi za shughuli za ujasiriamali; (skills)

Madawati ya uwezeshaji Wananchi yameanzishwa hadi katika ngazi ya Kata ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za dawati na kuleta ufanisi unaohitajika.

Uwezeshaji Wananchi kiuchumi unafanyika katika utaratibu wa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Katika kipindi cha Mwaka 2016/2017 – 2019/2020, Halmashauri imeweza kutenga na kutoa mikopo ya Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kukopesha wanawake, vijana na walemavu kwa uwiano wa 4:4:2 walio katika vikundi vinavyojihusisha na ujasiriamlai ili kuwaongezea nguvu ya mtaji na kuwakwamua kiuchumi.

Hadi sasa j -umla ya **Tshs. 678,974,062** zimetengwa kwenye bajeti ya Halmashauri na kutolewa kama mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali.

**Jedwali likionesha mikopo iliyotolewa kwa vikundi kwa Mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020**


| **Na.** | **Mwaka** | **Idadi ya vikundi vijana** | **Idadi ya vikundi wanawake** | **Jumla ya vikundi (ME + KE)** | **Mikopo kwa vijana (Tshs)** | **Mikopo kwa Wanawake (Tshs)** | **Jumla fedha za mikopo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **2016/2017** | 27 | 34 | **61** | 136,100.000 | 134,652,000 | **270,752,000** |
| **2** | **2017/2018** | 21 | 28 | **49** | 114,013,173 | 131,830,381 | **245,843,554** |
| **3** | **2018/2019** | 14 | 17 | **31** | 70,063,116 | 92,315,392 | **162,378,508** |
| **JUMLA KUU** | | **62** | **79** | **141** | **320,176,289** | **358,797,773** | **678,974,062** |






***GARI NDOGO YA ABIRIA ILIYONUNULIWA NA KIKUNDI CHA UMAMABAMKI, KILICHOPO KATA YA DUNDA***





***SHUGHULI ZA KIKUNDI CHA VIJANA CHA ARTIST AND TOUR GUIDE KATA YA DUNDA.***

**KIKUNDI CHA VIJANA CHA YATAKA MOYO - KATA YA MAGOMENI**




**TAARIFA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2015 - 2018**

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija na yenye kutatua kero za wananchi kwa fedha za mapato ya ndani, fedha za ruzuku toka Serikali kuu, pia michango ya wadau mbalimbali wa maendeleo.

Miradi hii imeendelea kutembelewa, kuwekewa mawe ya msingi, kukaguliwa na kuzinduliwa na Mwenge wa Uhuru kila Mwaka, hivyo Halmashauri imepokea Mwenge wa Uhuru na kuukimbiza katika miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya Halmashauri, katika kushiriki kwake, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kipindi cha miaka minne kuanzia 2015 hadi 2018 tumeweza kushika nafasi 2 kimkoa kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:-

**Matokeo ya Mbio za Mwenge wa Uhuru 2015-2019**

| **Mwaka** | **Kimkoa** | **Kikanda** | **Kitaifa** |
|---|---|---|---|
| 2015 | 2 | 11 | 62 |
| 2016 | 2 | 19 | 80 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2017 | 2 | 4 | 10 |
| 2018 | 2 | 3 | 3 |

**MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2018**



**Kikundi cha vijana Arts and Tour Guide, kilipotembelewa na Mwenge wa Uhuru 2018. Kitaifa 2019,**



**Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Ndg. Francis Kabeho akizindua Kituo cha Afya Kerege**



***Ukaguzi wa Kituo cha Afya Kerege 2018;***



***Uzinduzi wa kituo cha Afya Kerege 2018.***

***MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2019***



***Kituo cha Afya Kerege kilipotembelewa;***



***Shule ya Msingi Mshikamano - Zinga ilipokaguliwa na kuzinduliwa***



***Wakina mama wakipokea net za Mbu Toka kwa Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2019 Ndg. Mzee Mkongea Ally***



***Uzinduzi wa Ujenzi wa matanki ya Kuvunia maji ya mvua Kingani Seko***